**Learning by Ear – Hygiene: How to avoid diarrhoea**

**Episode 01 “Kukimbia”**

**Author** Njoki C. Muhoho
**Medical Advisor** Dr. Ngethe Muhoho
**Editor** Maja Braun
**Kisuaheli** Eric Ponda

| Scene | Characters | SAM – 17, m. |
|---|---|---|
| 1 | 1. MAMA SAM<br>2. MARIA<br>3. CHEMU<br>4. NARRATOR | MAMA SAM – 40, f.<br>MARIA – 43, f.<br>EDDI– 36, m.<br>DR SALLY – 34, f.<br>CHEMU – 15, f. |
| 2 | 1. SAM<br>2. CHEMU<br>3. NARRATOR | |
| 3 | 1. MAMA SAM<br>2. SAM<br>3. MARIA<br>4. BABY FATU | NARRATOR |
| 4 | 1. MAMA SAM<br>2. SAM<br>3. MARIA<br>4. CHEMU | |

**INTRO**

**MUSIC: THEME MUSIC**

**01. NARRATOR** Hujambo msikilizaji wa Deutsche Welle mahali popote ulipo na karibu kwa mfululizo wa vipindi vya LEARNING BY EAR, "Noa Bongo Jenga Maisha yako" tukizungumzia kanuni za Afya na kinga dhidi ya Ugonjwa wa kuhara. Visa vya ugonjwa wa kuhara vinazidi kuongezeka na kuwaua watu wengi hasa Barani Africa. Katika makala hii ya kwanza, tunakutana na SAM na Familia yake: Familia hii iko taabani, kwani, imazongwa na janga la ugonjwa wa kuhara. Kadhalika tunakutana na CHEMU, rafiki mkubwa wa Sam,na vile vile Jirani Maria Mamake Chemu. Maria ni Mtu wa majigambo na kimbelembele .

Na moja kwa hebu twende upande wa pili wa studio tusikie jinsi Sam, Familia yake, na Rafiki zake wanavyopambana na Ugonjwa huu wa Kuhara,chanzo, njia madhubuti za kinga na hata tiba.

**SCENE 1: SAM'S SCHOOL'S ATHLETICS FIELD.**

**02*. SFX: BACKGROUND CHEERING BY STUDENTS. FEET RUNNING.***

**03. MAMA SAM :** Kazana ….,kazana…. , ongeza mwendo SAM……, ongeza mwendo mwanangu … ongeza !

**04. CHEMU** : (***screaming at high pitch***) SAMu…! SAMu… !SAMu..

**05. MAMA SAM/CHEMU/MARIA:** SAMmu… SAMmu…. SAMmu… SAMmu…

**06. MAMA SAM:** ***(Excited)*** Huyo ni mwanangu…! Maria na Chemu hebu mtazameni !. mnaona Mwanangu anaelekea kushinda…..

**07. CHEMU** : Ooooh… na amependeza…!!

**08. MARIA :** Chemu, funga mdomo wako, wewe ni msichana mdogo sana kuanza kuwa na hisia kwa wavulana!

**09. MAMA SAM :** Ahh hata …..hata …kwa kijana wangu pia… ? Nilidhani sisi ni marafiki, Maria! Samu….. Samu.. ahhh hapana….! hapana ….! hapaaana …!

**10. CHEMU :** ***(horrified)*** Sam, sasa unafanya nini ?

**11. MARIA** Sasa ameanza tena... hata haikumchukua muda! Unaona sasa Chemu, si vizuri vile….. yule mvulana hawezi ku…

**12. MAMA SAM** Tazama….. Maria…!, sasa ameingia kichakani, kwani anaenda kufanya nini…. Kipi kinachoendelea ?

**13. MARIA** Kijana wako anatuonyesha vituko! Nani anayeweza kutoroka na kukimbilia msituni wakati anapoelekea kushinda mbio muhimu kama hizi?

**14. CHEMU** ***(sad)*** Sam amefanya nini ?

**15. MARIA** Kama unamjali sana Rafiki yako, mbona basi usiende kumjulia hali, kwanini kabadilika ghafla namna hii na kuanza kutuonyesha vioja. Nenda nenda upesi… hatuna muda wa kusubiri hapa !

**16. NARRATOR** **Ungemuona Sam kipindi cha mwezi mmoja uliopita, hungeutilia shaka uwezo wake wa kuibuka mshindi wa mbio hizi….!, lakini katika muda wa wiki chache tu zilizopita, Afya yake Sama imeanza kudhoofika . Nini**

**kinachomsumbua Sam?. Hebu tuungane na Chemu tufahamu kinachoendelea kichakani.**

**SCENE 2: IN THE BUSH – MARIA'S FARM**

***17. SFX: Birds, Crickets***

***18.*** **SAM :** *(**from some distance)** SIGHS OF PAIN AND FORCED BREATH*

**19. CHEMU :** *(**worried**)* Sam? Sam..? Uko wapi . Sam?

**20. SAM :** *(closer) SOUNDS OF SIGHS OF PAIN AND FORCED BREATH*

***21. SFX: Liquid splashing on ground***

**22. CHEMU :** SAM… Saaaam… ? Wacha mzaha wako Sam ..!

**23. SAM :** ***(strained voice)*** Niko… niko….. Hapa lakini usije karibu yangu! rudi…!

**24. CHEMU :** Toka huko basi, kwanini umeacha kukimbia, Kila mmoja sasa ana wasiwasi

**25. SAM :** *(**painfully**)* Nimekwambia usije huku, usije karibu yangu……! Rudi…. Rudi… haraka….!

**26. CHEMU :** Lakini kwanini umejiondo kwenye mashindano?

**27. SAM :** Hapana sijajiondoa bado nashiriki!

**28. CHEMU :** Wacha utundu wewe …. wewe…..! Umetoka mashindanoni na kukimbilia kichakani… kwani sasa …?Hebu toka upesi huko !

**29. SAM :** Siwezi, nilishindwa kwasababu tumbo lilianza kuniuma, tafadhali usije karibu nami!

**30. CHEMU :** Eeeeeeekkkk….. Uvundo wa nini huo, nini kilichooza hapa!

**31. SAM :** ***(a bit sarcastic)*** Nalinyunyuzia mbolea shamba la Mamako

**32. CHEMU :** (***Kidding, but also disgusted)*** SAMmmuuuu…..Kwani umeanza kuhara tena!

**MUSIC BRIDGE**

**NARRATOR** **Maskini Sam sasa yuko taabani. Aibu ilioje Mtu kujikuta katika hali hii akiwa na msichana anayempenda na kutaka kumfurahisha. Inashangaza jinsi Sam alivyoupata ugonjwa huu. Na je, ni wangapi katika Familia yake walioambukizwa ugonjwa huu? Hebu tuungane na Sam nyumbani kwao tusikie mambo yalivyo huko..**

**<u>SCENE 3: MAMA SAM'S HOME</u>**

***33. SFX: INTERMITTENT NOISES OF A BABY CRYING***

**34. MAMA SAM :** ***(anguished)*** Jamani… siamini….! nitafanya nini mimi? Maria hebu niambie nifanyeje. Mtoto wangu amenza kuhara…..! Mashaka gani yanayoiandama Familia yangu?.

**35. MARIA :** Nimekwambia mara nyingi. Kila mara umpikie mwanao Fatu uji mzito.Uji mzito hushika tumbo na kufayafanya maji mwilini kuwa mazito zaidi. Nitampikia uji mzito unaoshika sufuria. Hiyo ndio dawa ya kuhara…!.Lakini mkanye mwanao asiendelee kujisadia katika shamba langu!

***36. SFX: DOOR SLAMS: BABY FATU CRIES EVEN MORE***

**37. MAMA SAM :** Sam, tafadhali nisaidie kumshika huyu mtoto. Mshike na mimi ni …….

**38. SAM :** (***screams with disgust***) AAAHHH! Hebu angalia Fatu alivyonifanya, ameniharia mikononi na kulichafua shati langu pia

**39. MAMA SAM** Huyu ni mdogo wako….!.Na hata akikuchafua huwezi kupata madhara, isitoshe hii si mara ya kwanza hali hii kutokea. Shika kitambara hiki ujifute nacho na kisha ukitupe pale pembeni. .

**BRIDGE MUSIC**

**40. NARRATOR** Ugonjwa wa Kuhara, umeanza kusambaa katika nyumba ya Mama Sam. Kinyesi kipo kila mahali. Na bado wote wamesongamana jikoni. Je hii ndio sababu ya kuenea haraka kwa ugonjwa huu.? Familia hiyo huenda inaambukizana maradhi haya pasi na kufahamu. Lakini ipi hatima ya Mtoto Fatu? Anaonekana amezidiwa. Hebu tusikie iwapo watampeleka Hospitalini haraka.

**SCENE 4: MAMA SAM'S HOME**

***41. SFX: Door opening and slamming, intermittent baby cries***

**42. MARIA :** Chemu, weka huo uji pale (***exclaiming***) Sam, kwanini una mbeba Mtoto kama mkungu wa ndizi? Hebu mlete hapa nimnyweshe uji.

**43. CHEMU :** Mama, nakwambia uji mzito si dawa, Fatu anahitaji kupelekwa kwa Daktari.

**44. MARIA :** Wewe mtoto wa miaka 15 unaujuaje ugonjwa wa kuhara! Mtoto, Sam …..?

***45. SFX: Wet drip/dro p***

**46. SAM :** ***(hasty)*** Taratibu …. hana … ohhh hata sijamaliza kusema…...

**47. MARIA :** ***(disgust),*** Sasa hebu angalia umefanya nini, uvundo huu ni mkali kuliko….kuliko shimo la maji taka jijini.!

**48. MAMA SAM** Bibi aliniasia kwamba Mtoto akifanya hivyo ni baraka.

**49. MARIA :** Wangu alitumia maji matakatifu sio hiki kinyesi cha Mtoto. Sasa Chemu utanipa huo uji au la.?

**50. CHEMU :** Wacha!

**51. MARIA & MAMA SAM** Nini ?

**52. CHEMU :** Osha mikono yako kwanza!

**53. MARIA :** Kwanini?, mimi sijashika makaa …

**54. MAMA SAM** Chemu, Unafikiri tuna maji ya kuchezea kunawa mikono kila wakati?

**55. CHEMU :** Huyu Fatu amehara, na mwalimu anatushauri kila mara ni lazima kunawa mikono ili kujikinga na maambukiziyoyote..

**56. MARIA :** Nyamaza…!, huyu ni mtoto mdogo, sio kiwanda kinachotengeza kemikali za sumu .Sasa utamlisha au la.?

***57. SFX: Chair being pushed***

**58. MAMA SAM :**(***in surprise***) Sasa ni nini?

**59. SAM :** *(**in urgence** )* Nataka kujisaidia . *(Runs to the door)*

***60. SFX: Door being opened and slammed***

**61. CHEMU :** Ni tumbo lake linamuuma.Ameanza kuhara tena

**62. MARIA :** Nadhani anahitaji uji mzito pia. Chemu,hebu nenda nyumbani upesi ukapike uji mwengine.

**63. CHEMU :** Lakini bora tuwapeleke hospitalini.Mwalimu alisema….

**64. MARIA :** (**Angry**) Funga domo lako…! Mwalimu alisema hivi Mwalimu kasema vile. Huyu mvulana ni mvivu. Umechunguza, jinsi anavyopenda kuketi bure tu, hapendi kabisa kufanya kazi siku hizi.Hata kukimbia pia ameacha.

**65. MAMA SAM** Maria wewe ni rafiki yangu lakini humpendi mwanangu.Tafadhali muache tu. Huna shukrani.Katika muda wa wiki mbili hizi zilizopita amekuwa akikusaidia kunyunyuzia mbolea shambani….! mwako au unasahau?

**66. MARIA :**Nikitaka mbolea nitatumia kinyesi cha ngombe wangu sio huyu mtoto wako mvivu.

**67. MAMA SAM** Ni ya bure ….bila malipo…!

**68. MARIA :** Yananuka kila mahali hata kwenye mboga zangu.Sijui kwanini binti yangu Chemu anampenda. Kuanzia sasa sitaki kukuona na mazoea ya kufanya urafiki na mvulana asiyeweza kujizuia haja kubwa. Nani ajuaye,labda kuna mengi asiyoweza kuyazuia pia!.

**69. MAMA SAM** Maria utanisaidia na matatizo ya maradhi ya mtotto wangu…. au utaniongezea maudhi tu….!.

***70. SFX: BABY CRYING STOPS AND BABY FALLS ASLEEP***

**71. MARIA** *(**apologetic**).* Ah.. pole rafiki,unajua mimi ni kimbelembele Ha.haaa… Fatu amenyamaza au amelala?.Lakini hajakunywa uji wake, sivyo?.

**72. MAMA SAM** Mara nyingi huwa hivyo. Yeye ni kuhara tu… alie kisha akichoka alale, akiamka kazi ni hiyo hiyo. Hata siku hizi hali vizuri

**73. MARIA :** Hata anaonekana amepoteza nguvu nyingi mwilini…. amebadilika na hana siha tena!.

**74. CHEMU ;** Mwalimu wetu hutueleza kuwa uchafu husababisha ugonjwa wa kuhara.

**75. MAMA SAM** *(**shouting**)* Unasema nini wewe msichana….!. Eti nyumba yangu ni chafu?

**76. MARIA :** (***Shouting back***) Wee, usijaribu kumkaripia binti yangu, anasema tu vile anavyoambiwa na mwalimu shuleni.

**77. CHEMU :** Mwalimu husema kwamba ugonjwa wa kuhara husababisha Mtu kupoteza maji mwilini.

**78. MARIA :** Sasa, Chemu umeupata wapi werevu wote huo? Tunaweza kupata dawa kwenye kioski kilichoko karibu.

**79. CHEMU :** Anasema Mtu yeyote anayekwenda haja kubwa, zaidi ya mara nne kwa siku anapaswa kumuona Daktari haraka iwezekanavyo.

**80. MARIA :** **Sasa umeanza kunikera msichana wewe.**!

**81. MAMA SAM** Labda tupate ushauri zaidi kutoka kwa shemeji yangu Eddi na Mkewe Sallya ambaye ni Daktari. Hii ni kwa manufaa yetu sote!

**82. MARIA :** Aaahh sijali vyovyote vile!

**MUSIC BRIDGE**

**OUTRO**

**84. NARRATOR AMA KWA HAKIKA FAMILIA YA MAMA SAM INAKUMBWA NA HALI NGUMU.WATOTO WAKE WANAUGUA NAO USHAURI WA CHEMU AMBAYE ANAONEKANA KULIFAHAMU CHANZO CHA TATIZO HILO ANAENDELEA KUPUUZWA.NI MATUMAINI YETU KWAMBA MAMA SAM ATALIZINGATIA PENDEKEZO LA KUPATA USHAURI WA EDDI NA DKT. SALLY. JEE ATAYAZINGATIA HAYA YOTE NA JE, EDDI NA SALLY WATAWAHI KUTOKA JIJINI?**

**USIKOSE KUUNGANA NASI TENA KUFAHAMU YALIYOMO NA YALIYOMSIBU MTOTO FATU NA FAMILIA NZIMA YA MAMA SAM, KATIKA SEHEMU YA PILI YA MFULULIZO WA VIPINDI HIVI VYA LEARNING BY EAR: NOA BONGO JENGA MAISHA YAKO KUHUSU MARADHI YA KUHARA.**

NA JE WEWE UMEWAHI KUPATIKANA NA FEDHEHA YA UGONJWA HUU WA KUHARA? JE JANGA HILI LIMEWAHI KUKUABISHA MBELE YA MPENZI WAKO KAMA ILIVYOTOKEA KWA SAM?

UKIWA NA MAONI USISITE KUTUTUMIA NA PIA UKITAKA KUSIKILIZA TENA KIPINDI HIKI AU VIPINDI VINGINE UNAWEZA KUFANYA HIVYO KUPITIA MTANDAO WETU WA WWW.DW-WORLD.DE/LBE.

HADI WAKATI MWENGINE KWAHERI KWA SASA.